# ST. SCHOLASTICA NURSERY AND PRIMARY SCHOOLS

**IMESAJILIWA KWA** **FOMU**

**NAMBA : EM :15224**

**P.O. BOX 40570, UKONGA, DAR ES SALAAM - TANZANIA**

***[ The African Benedictine Sisters of St. Agnes – Chipole]***

**TEL: 0768 671859, 0759- 753493,0652-544901,0755-699121.**

**FOMU YA KUITWA KUJA KUFANYA USAHILI KWA WANAFUNZI**

**WATAKAOJIUNGA NA SHULE YA MT. SCHOLASTICA**

## A: MAELEKEZO MUHIMU

1. **GHARAMA YA FOMU NI : TSH. 20, 000 /=**
2. **ADA KWA WANAFUNZI WA SHULE YA AWALI KWA MWAKA NI TSH 950,000/=**
3. **ADA KWA WANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI DARASA LA I,II,III,V NA VI NI TSH 1,500,000/=**
4. **ADA KWA WANAFUNZI WA DARASA LA IV 1,650,000 /=**
5. **ADA PAMOJA NA MASOMO YA ZIADA KWA DARASA LA SABA NI TSH 1,850,000 /=**
6. **JAZA FOMU HII KWA USAHIHI, ANDIKA KWA HERUFI KUBWA TU.**
7. **KWA WANAFUNZI WAPYA WANAPASWA KUFIKA SHULENI NA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA NA PICHA MOJA YA (PASSPORT SIZE) SIKU YA KUFANYA USAHILI**

## B: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:

- Jina kamili______________________________Umri halisi______________Tarehe na Mwaka wa Kuzaliwa__________
- Darasa analoomba_________________________________________________
- Mahali anakotoka__________________Kata___________________Wilaya ______________Mkoa_______________
- Matatizo ya kiafya_____________________________________________________________________________
- Kabila____________________________Dini__________________________Dhehebu_______________________
- Jina la shule aliyotoka __________________________________________________Mwaka__________________

## C: TAARIFA BINAFSI ZA WAZAZI/MLEZI:

- Jina kamili la baba mzazi/mlezi___________________________________________________________________
- Jina kamili la mama mzazi/ mlezi_________________________________________________________________
- Simu ya baba mzazi/ mlezi_______________________________________________________________________
- Simu ya mama mzazi/ mlezi______________________________________________________________________
- Sanduku la barua_______________________________________________________________________________
- kazi ya baba mzazi /mlezi________________________________________________________________________
- kazi ya mama mzazi /mlezi________________________________________________________________________

**D:MUDA WA MASOMO**

- Muda wa kuwasili wanafunzi shuleni ni saa 1:00 asubuhi
- Masomo yanaanza saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri kwa shule zote za awali na msingi ***ISIPOKUWA*** Madarasa ya mitihani.

**E: MFUMO WA MASOMO YATOLEWAYO**

- Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Katika kipindi cha mwaka mmoja kutakua na mihula miwili, muhula wa kwanza Januari hadi Juni na muhula wa pili Julai hadi Desemba. Tunapokea watoto wenye umri kuanzia miaka 3 kwa watoto wa shule ya awali na umri wa miaka 6 na kuendelea kwa masomo ya shule ya msingi.

**F: UTARATIBU WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA : SHULE YA AWALI**

**MUUNDO WA ULIPAJI ADA KWA NURSERY**

| MALIPO | JANUARY | APRIL | JULY | SEPTEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| NURSERY(AWALI) | 400,000/= | 200,000/= | 200,000/= | 150,000/= | 950,000/= |

**G:UTARATIBU WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA: SHULE YA MSINGI**

**MUUNDO WA ULIPAJI ADA KWA DARASA LA 1,2,3,5 & 6**

| MALIPO | JANUARY | APRIL | JULY | SEPTEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| PRIMARY(MSINGI) | 600,000/= | 300,000/= | 300,000/= | 300,000/= | 1,500,000/= |

**MUUNDO WA ULIPAJI ADA KWA DARASA LA NNE (IV)**

| MALIPO | JANUARY | APRIL | JULY | SEPTEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| DARASA 4 | 1,000,000/= | 250,000/= | 200,000/= | 200,000/= | 1,650,000/= |

**ADA PAMOJA NA MASOMO YA ZIADA KWA DARASA LA SABA ITAKAYOANZA RASMI JANUARY HADI SEPTEMBA NI TSH: 1,850,000**

**MUUNDO WA ULIPAJI KWA DARASA LA SABA (VII)**

| MALIPO | JANUARY | APRIL | JULY | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| DARASA 7 | 1,000,000/= | 450,000/= | 400,000/= | 1,850,000/= |

**LIPIA KWA KUPITIA ACCOUNT NO ZIFUATAZO:**

1. **DCB ACCOUNT NO: 062010000002 ( ST.SCHOLASTICA NURSERY AND PRIMARY SCHOOL**
2. **CRDB ACCOUNT NO: 01J2031287600 (ST.SCHOLASTICA NURSERY SCHOOL**
3. **MKOMBOZI BANK ACCOUNT NO: 00120600570001 (ST.SCHOLASTICA NURSERY AND PRIMARY SCHOOL**

**MUHIMU: MWANAFUNZI YEYOTE HATAPOKELEWA AKIWA NA KIASI PUNGUFU ZAIDI YA MAELEKEZO YA ULIPAJI TULIYO YATOA**

**NB: ADA IKIISHALIPWA KWENYE AKAUNTI YA SHULE HAIRUDISHWI**

## H: USAFIRI NI NJE YA GHARAMA ZA ADA:

- Kuna chati maalumu inayoonesha gharama za usafiri kulingana na umbali wa vituo.

## I: MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ya St. Scholastica Nursery and Primary ipo <**KM (GARDEN) KIPUNGUNI B" KARIBU NA HOSPITALI MPYA YA MAGEREZA** Unapotokea Kariakoo shuka Madafu Mahakamani, **PANDA PIKIPIKI KUELEKEA KM** (**GARDEN).** Ukiwa unatokea kitunda shuka kitunda reline panda pikipiki kuelekea **KM (GARDEN).** Ukiwa unatokea kwa **MKOLEMBA**, kwa **DIWANI** au **MOSHI BAR** shuka **TRANSFORMA** panda pikipiki kuelekea **KM (GARDEN)** ndipo shule ilipo.Ukitokea **CHANIKA, PUGU,** shuka **MADAFU FUATA NJIA YA MAHAKAMANI.**

## J: SIKU YA KUFANYA USAHILI (INTERVIEW)

NB: Usahili (interview) unafanyika kila siku shuleni na kwa tarehe zilizopangwa isipokuwa siku ya Jumapili, hivyo kumbuka kuja na mtoto wako shuleni St. scholastica **KIPUNGUNI B" KM KARIBU NA HOSPITALI MPYA YA MAGEREZA ,Muda ni kuanzia Saa 3: 00 asubuhi.** Kumbuka pia kununua vifaa vya kuandikia kama vile kalamu ya wino, kalamu ya risasi (pencil), rula na ufutio.

## K: SHERIA ZA SHULE

**Kila mwanafunzi wa shule hii anapaswa kuzingatia yafuatayo;-**

**I.**Kuvaa sare za shule awapo darasani na popote anapokwenda nje ya shule hasa safari mbalimbali za kitaaluma.

**II.**Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika mazingira ya shule daima.Kibali maalum cha kutoka nje ya shule hutolewa na mkuu wa shule ,makamu wake au mwalimu wa taaluma kwa shida maalumu.

**III.**Ukosefu wa nidhamu wa aina yoyote iwe shuleni ama nje ya shule hautavumilika, hivyo mtoto atapewa adhabu na mwalimu wa darasa au mwalimu wa nidhamu au msaidizi wake.

**IV.**Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu viongozi wote, walimu wafanyakazi wazazi na wakuu wa shule.

**V.**Anapaswa kuwatii na kuwajali wenzake na wakubwa wote.

**VI.** Kazi ni sehemu ya elimu kwa hiyo, kila mwanafunzi lazima ashiriki kikamilifu katika kazi za kutunza mazingira kama kumwagilia maua, kufagia madarasa na mazingira ya shule.

**VII.** Mwanafunzi anapaswa kuheshimu wimbo wa Taifa, wimbo wa shule na nyimbo nyingine za uzalendo kama vile Tanzania nakupenda au tazama ramani.

**VIII.**Mwanafunzi awahi kila anapoitwa ama kusikia mlio wa kengele.

**IX.**Mwanafunzi awapo darasani anapaswa kujifunza kimya bila kelele.

**X.**Kashfa ya aina yeyote ile haitokubalika hivyo wazazi wake wataitwa kupewa taarifa ya kosa lililotendwa na mtoto wao.

**XI.**Matatizo madogo madogo yaanze kushughulikiwa kwanza na mwanafunzi kiongozi(kiranja) au mwalimu wa darasa au wa zamu au wanidhamu kabla ya kuyafikisha kwa mkuu wa shule. Hii haina haja ya kuficha makosa.

**XII.**Hairuhusiwi kutumia lugha chafu (matusi) au kupigana, atakayevunja sheria hii atafukuzwa shuleni.

**XIII.**Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa muungwana, mtiifu, mwaadilifu na mwajibikaji.

**XIV.**Utoro hautoruhusiwa kamwe. Mtoro atakuwa amejifukuza mwenyewe .

**XV.**Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni, mawasiliano yote hufanyika shuleni.

**XVI.**Hii ni shule ya Kikatoliki kwa hiyo Mwanafunzi wa dhehebu lolote anatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa na shule. Mwanafunzi atahudhuria kipindi cha Dini ya kikatoliki, kwa ajili ya kumjenga mwanafunzi kimaadili.

**L:. MWANAFUNZI ATAFUKUZWA SHULE IWAPO ATAPATIKANA NA MAKOSA KATI YA YAFUATAYO:-**

i) Utoro wa zaidi ya siku tano bila taarifa.
ii) Wizi/ kuiba.
iii) Kupigana na kutoa maneno ya kashfa.
iv) Ubaguzi wa kidini.
v) Uasherati.
vi) Ulevi wa aina yeyote( pombe,bangi au madawa ya kulevya).
vii) kuwa na mimba au kutoa mimba.
viii) Kurudia darasa moja mara mbili au zaidi.

## M. HESHIMA

Katika kusisitiza heshima kila mwanafunzi atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i) Kusimama na kumsalimia mwalimu ama mtu yeyote anayewazidi umri anapoingia darasani au kwenye mkutano.
ii) Wanafunzi waoneshwe umuhimu wa kushirikiana na kusaidiana katika kazi.
iii) Wanafunzi waelezwe umuhimu wa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kwao kama walezi wao.

iv) **Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:**
  a) Kuvuta sigara.
  b) Kufuga kucha na kuwa na nywele zisizo wekwa katika hali ya usafi.
  c) Kufuga ndevu.
  d) Kuvaa mavazi yasio na heshima( mini skirt).
  e) Kusuka nywele hasa watoto wa kike.

v) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya taifa na picha za viongozi wa serikali.
vi) Wanafunzi wazoeshwe kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma.
vii) Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa nguo za kidini kama vile hijabu ama kanzu wawapo shuleni.

## N: MUHIMU ZAIDI.

1. Unapokuja kuripoti shuleni uje na fomu hii.
2. Kama hutafika toa taarifa mapema.
3. **HATUTAMPOKEA MTOTO ASIYELIPIWA ADA.**

**NIMESOMA NA KUELEWA SHERIA ZA SHULE HIVYO NAAHIDI KUTEKELEZA KILA MOJA KAMA ZILIVYOAINISHWA**

**JINA LA MWANAFUNZI**______________________**SAHIHI**_________**TAREHE**_________

**JINA LA MZAZI**___________________________**SAHIHI**____________**TAREHE**__________

**JINA LA MWALIMU MKUU**______________________**SAHIHI**_________**TAREHE**_______

*Tushikamane, tushirikiane!!*
*Shule moja , familia moja!!*

--------------------------------------

**SR. POLYCARP NCHIMBI O.S.B**

**MWALIMU MKUU.**